

## **Maswali**

1. Yesu alizungumza na watu kwa mda gani?
2. Mwisho wa hiyo siku wanafunzi walimwambia Yesu nini?
3. Yesu aliwaauliza wanafunzi nini?
4. Filipo alisema watahitaji pesa ngapi?
5. Andrea alimwambia Yesu nini?
6. Yesu aliwaambia wanafunzi wafanye nini?
7. Kulikuwa na watu wangapi?
8. Yesu alifanya nini kabla ya kuwapa chakula?
9. Kila mtu alishiba chakula?
10. Vipande vilivyoachwa vilijaza vikapu vingapi?

## **Majibu**

1. Yesu alizungumza na watu kwa siku nzima mpaka jioni.
2. Wanafunzi walimwambia Yesu, "Watumé watu vijijini wajinunulie chakula."
3. Yesu aliwaauliza "Tutanunua chakula wapi ili hawa watu wale."
4. Filipo alisema watahitajika dinari mia mbili (pesa nyingi).
5. Andrea alipata kijana aliyekuwa na mikate 5 ya shayiri na samaki wadogo wawili.
6. Yesu aliwaambia wanafunzi waketishe watu.
7. Kulikuwa na watu kama elfu tano.
8. Yesu alishukuru Mungu kwa hicho chakula kabla awape watu.
9. Kila mtu alikula na kushiba.
10. Kulikuwa na vikapu kumi na viwili vilivyoja.

## **SHULE YA JUMAPILI YA CBM**



**Awamu ya 1 Mwaka wa 1**

# **38 Kulisha watu elfu tano**

## **Marejeo**

Matayo 14:13-21 na Yohana 6:1-14

## **Kiini cha somo**

Kuonyesha miujiza ya ajabu alizofanya Yesu na vile aliwajali watu

## **Maneno maalum**

1. Umati wa watu + Yesu + sikiliza + jioni + hakuna mkate
2. Nunua mikate + Filipo + mikate 5 + samaki 2
3. Keti chini + 5000 + nyasi
4. Vikapu 12 + vipande

**38.1** Alikokwenda Yesu umati mkubwa ulimfuata. Walimsikiliza akizungumzia juu ya Mungu na ufalme waajabu utakao kuja hapaduniani.

Siku moja alikuwa na m kutano mkubwa mno. Aliendelea kuwazungumzia na kuponya wagonjwa. Siku nzima walimsikiliza mpaka jioni na wanafunzi wakamjia Yesu.


Wakasema, "Hawana chakula na mda mchache giza kitaingia. Waache watu waende vijijini wanunue chakula."

**38.2** Yesu aliangalia huo umati mkubwa wa watu na akawahurumia. Akauliza Filipo, "Tutanunua mikate wapi ili wakule?"

Filipo alimuangalia kwa mshangao na kusema. "Mikate ya dinari mia mbili haitatosha kila mmoja apate kidogo."

Andrea, nduguye Petro, akamwambia, "Kuna kijana hapa mwenye mikate mitano na samaki wadogo wawili lakini haitoshi watu wote."

Yesu alitabasamu na akasema, "Waketisheni watu."



**38.3** Kulikuwa na nyasi nyingi pale kwa hivyo watu walikalia. Walikuwa kama watu elfu tano.

Yesu alichukuwa hiyo mikate ya shayiri na wale samaki wawili kutoka kwa kijana. Akashukuru Mungu kwa ajili ya hicho chakula, akavunja mikate na samaki kwa vipande na akawapa wanafunzi wake, nao wakawapa hao watu wote.

Kila mmoja alikula kiasi alichotaka. Wakashiba kwa hiyo mikate ya shayiri tano na samaki wadogo wawili.

**38.4** Walipomaliza kukula, Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Chukueni vipande vyote vilivyobaki, kisipotee chote chote."

Wanafunzi walitembea na kuokota kila kipande kilichobaki. Walijaza vikapu kumi na viwili kwa vile vipande vyta samaki na mikate vilivyoachwa.

Kila mtu alimwangalia Yesu, wakijua amefanya muujiza mkuu.

Lazima ye ye ndiye mfalme, Mwana wa Mungu.